




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA



Kumb.Na. **MDC/ADM/10/30/VOL 1/91**

25/05/2023

YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Maswa imepata idhini ya kutekeleza Ikama na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kupitia barua **Kumb. Na.FA.97/228/01"TEMP"/06** ya tarehe **06/Aprili,2023** iliyotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Maswa anatangaza nafasi za kazi ya **Mtendaji wa Kijiji Daraja la III** kwa Masharti ya kudumu, Hivyo Watanzania wote wenye sifa hizo mnakaribishwa kutuma maombi ya kujaza nafasi hizo kama ifuatavyo:-

1.1 MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI 02

Sifa za Mwombaji: -

- (i) Wahitimu wa kidato cha nne au sita wenye cheti cha [NTA Level 5] au Certificate katika moja ya fani zifuatazo
- (ii) Utawala
- (iii) Usimamizi wa Rasilimali watu
- (iv) Maendeleo ya Jamii, Sheria, Usimamizi wa Fedha au
- (v) Sayansi ya Jamii kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali
- (vi) Awe na umri usiozidi miaka 45
- (vii) Awe na cheti cha kuzaliwa.

1.2. MAJUKUMU YA KAZI

- (i) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- (ii) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika kijiji.

- (iii) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- (iv) Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- (v) Kutafasiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- (vi) Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji Mali.
- (vii) Kiongozi wa Wakuu wa vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- (viii) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- (ix) Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
- (x) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na Migogoro ya Wananchi.
- (xi) Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji.
- (xii) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.
- (xiii) Kazi nyingine utakazopangiwa na Mwajiri.

1.3 NGAZI YA MSHAHARA

Mshahara: Ngazi ya **TGS B** kwa mwezi.

2.0. MASHARTI YA JUMLA

- Awe raia wa Tanzania.
- Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45
- Waombaji waambatanishe nakala za cheti cha kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo na vyeti vya kidato cha nne vilivyothibitishwa na Wakili au Mahakama.
- Awe na kitambulisho Taifa (NIDA)
- Muombaji ambatanishe picha mbili [2] ndogo ya rangi [passport size] ya hivi karibuni.

- Testimonials, Provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita [form VI and form IV result slip] **HAVITAKUBALIWA.**
- Waombaji ambao wapo kwenye Ajira, barua za maombi zithibitishwe na Waajiri wao.
- Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kwa Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

3.0. UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya wilaya ya Maswa,
S.L.P. 170,
MASWA –SIMIYU.

Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe 02.06.2023 Saa 9.30 Alasiri.**

NB:

Tangazo hili linafuta tangazo la kazi lenye Kumb.Na. MDC/ADM/10/30/VOL.I/90 la tarehe 17 Aprili,2023 Nafasi Mtendaji wa Kijiji Daraja la III nafasi (10). Aidha tangazo hili linapatikana kwenye tofauti ya www.ajira.go.tz na katika mbao za matangazo za Halmashauri na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu.


Simon Berege
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
MASWA